# Mchango wa Kazi Teule za Fasihi katika Kukabiliana na Janga la UKIMWI

*Charles Kituni Wasike, Mosol Kandagor* na *S. M. Obuchi*
*Chuo Kikuu cha Moi*

**Ikisiri**

**Janga la UKIMWI limekuwa katika jamii zetu kwa zaidi ya miaka thelathini. Katika kipindi hicho zaidi ya watu milioni 34 wameambukizwa ugonjwa huo ulimwenguni. Isitoshe, kwa mujibu wa UNAIDS (2012), zaidi ya watu milioni 18 wameaga dunia. Tangu kisa cha kwanza cha UKIMWI kugunduliwa nchini Kenya, juhudi mbalimbali zimefanywa kujaribu kupunguza idadi ya visa vya maambukizi mapya. Juhudi hizo ni pamoja na kuelimisha umma kuhusu mbinu na njia mbalimbali za kujikinga dhidi ya maambukizi. Njia moja muhimu ambayo yaweza kutumiwa kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu UKIMWI ni kupitia kazi ya fasihi. Kwa mintarafu hiyo, makala haya hususan yanatathmini mchango wa kazi teule za fasihi andishi katika kukabiliana na janga la UKIMWI. Kwa vile tiba ya UKIMWI haijagunduliwa, utafiti huu ulilenga kutoa mchango kwa jamii ambao waweza kufahamisha umma kuhusu mbinu na njia za kutumika katika kukabiliana na janga la UKIMWI.**

**Maneno muhimu:** Maradhi, Dhamira, UKIMWI, Unyanyapaa

## Utangulizi

Tangu kugunduliwa kwa maradhi ya UKIMWI katika miaka ya 1980 nchini Kenya, jamii imeendelea kuhamasishwa kuhusu jinsi ya kukabiliana na maradhi haya. Baadhi ya makundi yaliyojishughulisha ni kama vile mashirika ya kibinafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali, wanahabari, wanamziki, viongozi wa kisiasa, asasi za kidini na wasomi. Waandishi mbalimbali wameshughulikia mada ya UKIMWI kupitia tanzu mbalimbali za fasihi. Mutembei (2009) anaeleza fasihi kama kiashiria katika kupambana na UKIMWI. Anasema kwamba katika fasihi, matumizi ya tamathali za usemi kama vile sitiari, tashbihi, tashhisi na hata kejeli ni kichocheo kikubwa katika kuelezea na kueneza kampeni dhidi ya kuenea kwa UKIMWI.

Kazi mbalimbali za fasihi aghalabu hujishughulisha na masuala anuwai yatokeayo katika jamii kiuchumi, kisiasa na kijamii. Wasanii wa kazi hizo huwasilisha ujumbe kwa madhumuni ya kuifunza jamii, kuionya na kuielekeza kwenye njia sahihi. Waandishi wengi wa kazi za fasihi wamejishughulisha na dhamira ya ugonjwa wa UKIMWI kwa ajili ya kuielimisha jamii ili iweze kuchukua hatua stahiki za kuepukana na janga hili. Makala haya yanahakiki baadhi ya maandishi teule ili kutathmini mchango wao katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI. Fasihi ni kati ya njia zinazotumiwa kama jukwaa la kuhamasisha jamii kuhusu masuala yanayowazingira watu. Ni kutokana na kugundua umuhimu wa fasihi katika jamii ambapo Taasisi ya Ukuzaji Mitalaa, Kenya imependekeza kuwa mada kuhusu masuala ibuka yakiwemo UKIMWI yazingatiwe katika fasihi kutoka darasa la kwanza hadi kidato cha nne. Vilevile ni somo la lazima kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa Chuo Kikuu. UKIMWI umejitokeza katika tanzu mbalimbali za fasihi kama vile ushairi, riwaya, hadithi fupi na tamthilia.

Dhamira ambayo sasa imejisimika na kuwa na mizizi katika jamii ni ile inayojadili ugonjwa wa UKIMWI. Nyimbo, mashairi, ngonjera na michezo ya kuigiza ilianza kulizungumzia janga hili hasa kutokea mwishoni mwa miaka ya 1980 kulingana na Mutembei (2001 na 2002). Kwa sasa nyimbo mbalimbali kuhusu UKIMWI, madhara yake na hasa jinsi ya kuepukana nayo zinaimbwa katika maeneo mengi. Utafiti wetu unatathmini mchango wa maandishi hayo katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI. Utafiti huu umechochewa na sababu kwamba kufikia sasa, ugonjwa wa UKIMWI hauna tiba na hivyo basi njia mbadala ya kuendeleza uhamasishaji wa jamii ni kupitia maandishi teule ya fasihi.

Katika kazi hii, tulihakiki kazi za tanzu tatu za fasihi andishi: riwaya, tamthilia na hadithi fupi zilizoteuliwa kimakusudi ili kupata data iliyotosheleza mahitaji ya utafiti. Uteuzi wa sampuli iliyotumiwa katika utafiti huu ulikuwa wa kimaksudi na ulihusisha riwaya zifuatazo: *Sitaki iwe Siri* (Matundura, 2008), *Ua la Faraja* (Mkufya, 2005), *Pendo Katika Shari* (Momanyi, 2008) na *Kala Tufaha* (Omar, 2007). Tamthilia zilizoteuliwa zilikuwa: *Giza* (Jilala, 2004), *Kilio Chetu* (Medical Aid Foundation, 1995) na *Orodha* (Reynolds, 2006). Hadithi fupi zilizotumika zilikuwa: *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* (Iribemwangi, (2007), *Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine* (King'ei na Kobia, 2007) na *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine* (Walibora na Mohamed, 2007).

## Mchango wa Kazi Teule za Fasihi Katika Kukabiliana na UKIMWI

Katika sehemu hii tumechunguza namna maandishi teule yanavyojadili namna ya kukabiliana na maradhi ya UKIMWI pamoja na kuwaonya wahusika kuhusu mienendo inayoweza kusababisha maambukizi. Baadhi ya maandishi pia

yanawapa moyo waathiriwa wa ugonjwa wa UKIMWI kwa kuwapa matumaini ya kuweza kuendelea kuishi maisha ya kawaida.

Wakati wote msimulizi huwa na dhamira au mwelekeo fulani anaokusudia msikilizaji au msomaji wake kuupata. Katika uhakiki wa matini, Genette (1980) anaeleza kwamba ni vyema kuweza kutambua yafuatayo katika kazi yoyote, kwamba: ni nani anaona, nani anawakilisha mtazamo wa msimulizi na nani anayezungumza. Tukizingatia kauli hii, mtazamo wa msimulizi umetuwezesha kuchunguza kusudi la masimulizi haya kama yenye lengo la kuonya wale ambao hawajapata maradhi ya UKIMWI kuepukana na mienendo inayoweza kuwaingiza katika janga hili. Aidha, maandishi haya yanapendekeza njia ya kufanya mapenzi salama ya kumwezesha mhusika kuepuka maambukizi. Aidha, mtazamo huo umetuwezesha kuona njia za kuwafariji wahusika walioathiriwa kwa kuwapa matumaini ya kuishi maisha ya kawaida. Sehemu ifuatayo inafafanua mambo haya kwa kina.

**Kuepukana na Uasherati**

Waandishi mbalimbali katika maandishi teule wanaionya jamii dhidi ya uasherati kama njia kuu ya kueneza maradhi ya UKIMWI. Katika riwaya ya ***Ua la Faraja***, msanii anaionya jamii dhidi ya uasherati kama njia inayoeneza maradhi ya UKIMWI. Katika riwaya hiyo, mhusika Queen alikuwa mwanamke mashuhuri mtaani kwa urembo wake, msomi na mwenye cheo kikubwa kazini. Ingawa hivyo, mwanamke huyo hakujiheshimu kwa kuwa alifanya mapenzi na wanaume wengi kama vile Ngoma na Omolo.

Ingawa mhusika Queen alikuwa mtu mashuhuri katika jamii, aliharibu umaarufu wake kwa kushiriki uzinzi. Msanii anasema, "*Ni kweli kwamba mwanamke yule malaya amewajeruhi watu aliowapenda kiasi kile? Kama amedhuru Ngoma, basi hata dada yake amedhurika. Na kama hao wamedhurika, Omolo je, atakuwa amepona? Asubuhi ya usiku ile, Queen ndiye aliyepiga simu na kumwambia ana jambo la muhimu kumwambia Omolo. Pengine jambo lenyewe ni hizo habari za UKIMWI! Uk. 59-60"* Katika riwaya ya *Ua la Faraja*, twaelezwa namna ambavyo Queen alitaka kufanya mapenzi kwa lazima na Omolo. Ilibidi atumie ujanja wa kuweka dawa ya kuamsha hisia ya mapenzi kwa kinywaji cha Omolo ndipo akafaulu.

Katika riwaya ya *Ua la Faraja*, mhusika mwingine aliyekuwa malaya pale Tandika alikuwa Asha. Asha Mmayema alikuwa na rafiki Mzungu aliyeitwa Hastings. Kabla ya kifo chake, Hastings alimjengea Asha nyumba nzuri ya ghorofa na kumwachia pesa nyingi. Baada ya kifo cha Hastings, Asha hakutaka kuolewa na kwa sababu alikuwa na mali, hakutaka kujifunga katika ndoa. Asha alikuwa na pesa zilizomfanya kuwa na uhuru wa kuwanunua wanaume.

Uhuru wa Asha unampa kibali cha kushiriki mapenzi na Ngoma. Kutokana na uhusiano huu, Asha anapata UKIMWI kwa vile Ngoma alikuwa rafikiye

Queen ambaye alikuwa ameambukizwa UKIMWI. Mwandishi anasema, "*Msafiri akanyanyuka kwa nguvu na kutaka kumwendea pale alipo. Macho yake yalikuwa mekundu kwa shauku."* (Ua la Faraja uk. 81). Kutokana na tabia na mienendo ya Asha tunaona maradhi haya yakiingia moja kwa moja katika ndoa ya Msafiri. Kwa mintarafu ya matukio haya, msimulizi anatahadharisha dhidi ya kushirikiana na wanawake malaya kama vile Queen na Asha. Iwapo wanaume watajihusisha na wanawake kama hawa, ni vyema, kutumia mipira ya kondomu kama alivyofanya Omolo. Omolo alilala na Queen lakini akatumia mipira na hivyo akaepuka kuambukizwa maradhi ya UKIMWI. Ujumbe wa mtunzi ni kwamba, jamii inapaswa kukomesha mienendo na tabia ya uzinzi wa wahusika kama vile Asha ili iepukane na maenezi na usambazaji wa ugonjwa wa UKIMWI.

Katika riwaya ya *Kala Tufaha*, mtunzi pia anatuonyesha wahusika ambao walijihusisha na uasherati. Msanii anatueleza kuwa mhusika Fumbwe alishiriki uasherati sana baada ya kutengana na mke wake Hatima. Mtunzi anatueleza kuwa Fumbwe alifika mahali akawa mtu asiyepisha rinda kumaanisha kuwa alikuwa anafanya mapenzi kiholela. Mhusika Fumbwe anapofumania mke wake Hatima, aliamua kujiingiza katika ulevi pamoja na kufanya mapenzi na wanawake wengi na mwishowe kupata ndwele isiyotibika. Kauli hii inathibitika kutokana na tabia za Fumbwe ambaye anafanya mapenzi na wasichana wadogo hata ofisini. Mwandishi anapoiangazia tabia ya Fumbwe, anawatahadharisha wanawake kutojihusisha na wanaume wenye wapenzi wengi kwa vile tendo hili laweza kusababisha wapate maradhi ya UKIMWI. Kutokana na mifano hii, wasanii wanaonya dhidi ya uasherati kama njia mojawapo ya kujiepusha na maradhi ya UKIMWI. Ni wazi kuwa wahusika wengi wanaoambukizwa maradhi ya UKIMWI katika riwaya zilizotajwa wanashiriki katika uasherati unaowaletea maangamizi hatimaye.

Katika riwaya ya *Pendo katika Shari*, mwandishi anasawiri maisha ya mhusika Sulubu ambaye alimdhulumu mkewe kwa kujiingiza katika kufanya mapenzi kiholela. Hata marafiki wa Sulubu wanashuhudia kwamba Sulubu hakuwa mwaminifu katika maisha yake ya ndoa. Licha ya ushauri ambao Sulubu alipewa na marafikize, aliwapuuza na kuendelea na tabia yake ya uzinifu.

Mwandishi anaionya jamii dhidi ya kujihusisha na wapenzi wengi na kufanya nao mapenzi kiholela. Mtunzi anasema, "*Sulubu, mimi nakujua vizuri sana. Wewe una wapenzi chungu nzima na wengine hata huwajui majina yao. Kwa hivyo, huwezi kujua ni yupi atakayekuambukiza maradhi baadaye. Leo una Amina, kesho kwa Cheupe, kesho kutwa kwa Rosa. Huoni unajitia kitanzi? Unajua UKIMWI unaua maelfu ulimwenguni lakini unafikiri wewe huwezi kuwa mmoja wa hao maelfu?"*(Pendo katika Shari, uk. 30). Twaelezwa na msanii kuwa Sulubu alikuwa na wapenzi ambao hakuwajua baadhi yao kwa majina. Zaidi ya hayo alikuwa anawabadilisha kama nguo na hangejua ni yupi ambaye angemuambukiza UKIMWI. Hatimaye, Sulubu alipata maradhi ya UKIMWI

kisha akawaambukiza wake zake. Wanawake wote pamoja na mtoto Pendo walifariki baada ya kupata UKIMWI. Sulubu mwenyewe hatimaye alifariki kutokana na maambukizi ya maradhi haya.

Mtunzi anapendekeza matumizi ya kondomu, uaminifu wa mapenzi, ufahamu na uelewa, uadilifu na uwajibikaji kama njia bora za kupambana na ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi ana msimamo kwamba njia bora ya kupambana na ugonjwa wa UKIMWI ni kuepukana na tabia za uasherati ambazo zinakiuka maadili ya jamii. Licha ya kuepuka uasherati kwa kuzingatia maadili mema ya jamii, wasanii katika kazi zilizoteuliwa katika utafiti huu wamependekeza matumizi ya mipira ya kondomu kama njia ya kupambana na UKIMWI.

**Matumizi ya Mipira ya Kondomu**

Waandishi wa kazi teule zilizotumiwa katika utafiti huu wanaangazia matumizi ya mipira ya kondomu kama njia bora ya kuepuka kuambukizwa maradhi ya UKIMWI. Katika riwaya ya *Ua la Faraja*, mwandishi kupitia mhusika Jose anaonyesha namna ambavyo matumizi ya kondomu ni muhimu katika kuepuka maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI. Jose alifanya kazi ya kuhamasisha watu kuhusu matumizi ya 'soksi' au kondomu na ndiyo sababu pia alikuwa akifanya biashara ya kuuza kondomu katika baa ya Malaika kila jioni. Kupitia Jose, mwandishi anasisitiza matumizi ya mipira ya kondomu katika kufanya ngono. Mtunzi anasema, "*Mambo kwa soksi! Mambo kwa soksi! Maji uyavulie nguo ndipo ukayaoge! Ulapo ndizi usiimenye ila ivishe gando*." (Ua la Faraja, uk. 12). Msanii anasema kuwa ukitaka kula ndizi, usiimenye ila uivishe gando. Aidha anaongeza kuwa mtu akitaka kuifurahia ngono salama hana budi kuvaa mpira au kondomu. Dhana ya kuvishana mipira inafaa kuwa jukumu la watu wote iwapo wanajamii wangetaka kufanikiwa katika vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI. Katika jamii kuna watu wengi ambao hawapendi kuvaa mipira ya kondomu wanapofanya mapenzi kwa kuwa wanaamini kwamba raha ya kufanya ngono inapungua wakati mtu anapotumia mipira hiyo. Wazo hili linashadidiwa na mtunzi wa tamthilia ya *Kilio Chetu* kupitia mhusika Joti. Joti anajidai vile alivyompeleka msichana katika gesti ya Msomali na kufanya mapenzi. Anasema, "*Shiti wewe. Nini kondomu bwana! Pekepeku tu... Unaweza kula pipi na ganda lake wewe?"*(uk. 18). Ni bayana kutokana na dondoo hili kwamba vijana hawakufurahia kutumia mipira ya kondomu. Matokeo yake yalikuwa kwamba Joti hatimaye aliambukizwa ugonjwa wa UKIMWI.

Kulingana na Kathenya (2002), serikali na wanajamii wanafaa kusisitiza uaminifu katika uhusiano na wala si matumizi ya mipira ya kondomu. Maoni ya viongozi wa Kanisa la Katoliki ni mazuri lakini hayawezi kuwa ya uhalisia katika jamii ya kisasa. Ingawa walio katika ndoa wanaweza kujaribu kuwa waaminifu, ni takriban asilimia mia moja tu ambao watakuwa waaminifu. Kwa hivyo, wale

ambao wanakosa uaminifu wanaweza kuepuka UKIMWI ikiwa watatumia mipira wakati wa kufanya ngono. Isitoshe, kuna vijana wengi ambao hawajaoa na ni vigumu sana katika jamii ya sasa kusema kuwa vijana wote watajitunza na kutojihuisha na kufanya mapenzi kabla ya ndoa. Ukweli ni kuwa vijana wanaofanya mapenzi kabla ya ndoa ni wengi kuliko wale wanaojitunza. Hivyo basi pana haja ya kuihamasisha jamii kutumia mipira ya kondomu kama njia ya kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI.

**Uwazi Kuhusu UKIMWI**

Vita dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI vitafaulu tu iwapo jamii itakuwa na uwazi katika kuuzungumzia ili kupata maelezo ya kutosha kuuhusu. Katika riwaya ya *Sitaki Iwe Siri*, mwandishi anaisawiri jamii ikijaribu sana kuuficha ukweli kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Nyanya Mwalonga alijaribu sana kuwaficha wajukuu wake kuhusu maradhi yaliyowaua wazazi wao. Alikuwa na hofu kuu kuwafahamisha ugonjwa uliomuua mtoto wake Matano na mke wake. Ugonjwa wa UKIMWI uliogopwa na haungetajwa tu kwa uwazi hadharani. Kitendawili cha kifo cha wazazi wa Musa kilimchochea afanye utafiti wa ugonjwa wa UKIMWI.

Musa alishiriki katika shindano lililoandaliwa na Shirika la Afya Ulimwenguni pamoja na Wizara ya Afya kuadhimisha siku ya UKIMWI ulimwenguni. Katika shindano hilo, Musa aliibuka mshindi kwa kuandika insha nzuri sana kuhusu mada ya *Sitaki Iwe Siri*. Hii ina maana kwamba ugonjwa wa UKIMWI haukustahili kuwekwa kama siri kinyume cha mawazo ya nyanya Mwalonga. Nyanya anakiri kwamba alitaka kuwaficha wajukuu wake kuhusu chanzo cha vifo vya wazazi wao lakini mwandishi anasema kuwa nyakati za kuuficha ugonjwa wa UKIMWI zilikuwa zimepita.

Nyanya Mwalonga anakiri kuwa aliwaficha wajukuu wake siri ya ugonjwa ambao uliwaua wazazi wake. Anakiri kwamba alitaka ugonjwa uliowaua Matano na mke wake ubakie siri. Msanii anasema, "*Ni sadfa kwamba siri niliyoighubika kwa miaka mingi ili wajukuu zangu wasiijue imefichuliwa. Wajukuu wangu hawa ni mayatima. Wazazi wao walifariki kutokana na maradhi ya UKIMWI, nao wakabaki mikononi mwangu. Waliponiuliza kilichowaua wazazi wao, niliwajibu kuwa ni maradhi. Nilitaka iwe siri lakini sasa Musa huyu ameandika insha ya ushindi. Sitaki Iwe Siri. Hii ni hatua muhimu katika vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI*…"(Sitaki Iwe Siri, uk. 66). Mwandishi anatueleza kutokana na dondoo lililonukuliwa kwamba njia nyingine ya kukabiliana na maradhi ya UKIMWI ni kuwa wazi kuyazungumzia.

Jamii inapokuwa na uwazi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI, itauelewa zaidi na hivyo itachukua hatua za tahadhari kuuepuka. Lakini mtazamo wa wanajamii kama wa nyanya Mwalonga wa kuuficha na kutouzungumzia ugonjwa huu inauendeleza ugonjwa wa UKIMWI badala ya kuuzuia. Hii inatokana na sababu

kwamba watu wasipouzungumzia na kuuelewa zaidi ugonjwa huu, watazidi kuathirika nao. Hivyo basi mwandishi wa riwaya ya *Sitaki Iwe Siri* anasisitiza kuwa njia bora ya kupambana na ugonjwa wa UKIMWI ni kwa kuufanyia utafiti sawa na alivyofanya Musa na kuuweka wazi na kuuzungumzia kwa uhuru badala ya kuufanya uwe siri. Kwa ujumla, mwandishi anapendekeza kwamba wanajamii wakubali kwamba ugonjwa wa UKIMWI upo na bado tiba yake haijapatikana. Katika tamthilia ya *Giza,* mwandishi anatueleza kwamba njia bora ya kupambana na maradhi ya UKIMWI ni kuwa wazi na kutoficha chochote kinachofungamana na maradhi haya.Mwandishianatuonyesha namna ambavyo jamii bado inauficha ukweli kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Mtunzi anasema, "*Mmesikia! Haya UKIMWI ni kwa maskini. Wakubwa, viongozi hawaugui UKIMWI ila shinikizo la damu, Kansa na kufa ghafla. Jamii hii inakwenda wapi? Nani atasema Wazi ana UKIMWI ili jamii ione na ijifunze, tutazaa watoto Wenye UKIMWI mpaka lini?"* (Giza, uk. 22).

Katika jamii inayorejelewa, ni watu maskini ambao husemekana wamekufa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Watu mashuhuri na hasa viongozi wanapofariki kutokana na UKIMWI, jamii haiko tayari kukubali kuwa wamekufa kutokana na UKIMWI. Jamii zao hutangazia waombolezaji kwamba marehemu amefariki kutokana na magonjwa mengine kama vile shinikizo la damu, malaria au ugonjwa wa moyo lakini si UKIMWI. Matendo kama haya yanaficha ukweli kuhusu UKIMWI na hivyo kuufanya uendelee kuangamiza maisha ya watu katika jamii. Mwandishi ana msimamo kuwa njia bora ya kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI ni kuwa wajasiri na kutangaza hadharani kwamba fulani amefariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Uwazi huu unaweza kuchangia pakubwa katika kukabiliana na maradhi ya UKIMWI.

Mwandishi wa tamthilia ya *Orodha* anapendekeza wanajamii wawe wazi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Anasema kuwa iwapo mtu amefariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI, jamii iwe tayari kutangaza hivyo bila kuficha na kuyasingizia magonjwa mengine kuwa chanzo cha kifo. Katika tamthilia ya *Orodha,* mwandishi anatuonyesha upinzani uliotoka kwa wanajamii wakati ambapo Mama Furaha alipotaka kusema ukweli kuhusiana na kifo cha mtoto wake. Msanii anasema, "*Na katika jina la Mungu, ukweli ni lazima usemwe! Yeye si wa kwanza wala hatakuwa wa mwisho iwapo hatutaukubali ukweli! Marafiki zangu, ndugu zangu wanakijiji… lazima tukumbuke kwamba Furaha aliteseka kutokana na virusi hivi vya kutisha..."* (Orodha, uk. 3). Mama Furaha hakutaka kuficha chochote kuhusiana na kifo cha bintiye. Alitangaza hadharani kuwa alikufa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI jambo ambalo halikupokelewa vyema na baadhi ya wanajamii.

Inasikitisha kuwa hata Padri James hakutaka uwazi usemwe kuhusu kifo cha Furaha kwa kuwa aliwahi kufanya mapenzi naye. Katika siku ya mazishi, Mama Furaha alijaribu akasoma ile orodha na kutangaza wazi kuwa mwanawe alikufa

kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Ukweli ukisemwa, jamii itatambua namna ugonjwa wa UKIMWI unavyoangamiza watu na hivyo kuchukua tahadhari kuepukana nao. Pia katika kufanya hivyo, jamii itapata changamoto na kuchukua tahadhari kuepukana na mienendo inayoweza kuhatarisha afya na maisha ya watu. Pamoja na uwazi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI, uaminifu katika maisha ya ndoa ni muhimu kwenye vita dhidi ya UKIMWI.

**Uaminifu Katika Maisha ya Ndoa**

Wasanii mbalimbali wanatueleza kwamba njia nyingine ambayo inaweza kutumika kuyafanya maradhi ya UKIMWI kudhibitika ni wanajamii kuwa waaminifu katika maisha ya ndoa. Katika riwaya ya *Ua la Faraja*, Ngoma na Msafiri wanawaambukiza wake zao UKIMWI kwa kuwa hawakuwa waaminifu katika maisha yao ya ndoa. Ngoma alikuwa mume wa Tabu lakini alikuwa akifanya mapenzi na Queen aliyekuwa mwanamke mzinifu. Ngoma alipata maradhi ya UKIMWI na kumwambukiza mkewe Tabu. Aidha, Ngoma alifanya mapenzi na Asha na kumfanya Msafiri aliyekuwa mpenzi wa Asha kuambukizwa. Omolo alijua haya na alipokuwa Malaika Bar, aliwaona Ngoma na Asha wakizozana. Vilevile Ngoma na Asha walikuwa na uhusiano wa kimapenzi. Hii ina maana kuwa mhusika Ngoma alikuwa katika uhusiano wa kimapenzi na wanawake wengi sana. Msanii anatueleza, "*Ngoma na Asha walikuwa na uhusiano wa kimapenzi. Pia, Omolo alikwishawahi kumfumania Ngoma nyumbani kwa Queen. Alikuwa anaijua tabia ya uzinzi ya jirani yake. Ikiwa Queen alikuwa mgonjwa, bila shaka amemwambukiza Ngoma kama hawakutumia mipira. Je, mzozo ule unahusiana na yale aliyoyakuta Queen siku ile?*" (Ua la Faraja, uk.71). Katika muktadha huu, msanii antufahamisha kwamba Queen alikuwa anaugua ugonjwa wa UKIMWI. Ikiwa Queen alikuwa anaugua ugonjwa wa UKIMWI, bila shaka alimwambukiza Ngoma na wakati huo huo iwapo Ngoma alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Asha, bila shaka alimwambukiza. Kwa upande mwingine, Asha naye alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Msafiri na hivyo basi kumuambukiza. Ni wazi kwamba ingawa Ngoma alikuwa ameoa hakuwa mwaminifu na ndiyo sababu ilimfanya kumwambukiza mke wake UKIMWI. Alifanya mapenzi na Queen na Asha bila kutumia mipira.

Katika riwaya ya *Pendo Katika Shari*, mwandishi anamchora mhusika Sulubu kama mfano wa watu katika jamii ambao walikosa kabisa uaminifu katika maisha yao ya ndoa. Sulubu alikosa uaminifu ambao ulisababisha akapata maradhi ya UKIMWI. Licha ya kutahadharishwa na marafikize, Sulubu aliwapuuza na kuendelea tu na tabia yake ya uzinzi ambayo hatimaye ilimletea madhara. Sulubu alikuwa na wapenzi wengi hata wengine ambao hukuwajua kwa majina. Sulubu alikuwa anawabadilisha wanawake kama nguo.

Mwandishi antueleza, "*Sulubu mimi nakujua vizuri sana. Wewe una wapenzi chungu nzima, na Wengine huwajui hata majina yao. Kwa hivyo, huwezi kujua ni yupi atakayekuambukiza maradhi baadaye. Leo una Amina, kesho una Cheupe, kesho kutwa kwa Rosa. Huoni unajitia kitanzi? Unajua UKIMWI umewaua maelfu ulimwenguni lakini unafikiri wewe huwezi kuwa mmoja wa hao maelfu."*(Pendo Katika Shari, uk. 30). Sulubu alitahadharishwa na rafikiye kuhusu hatari ya tabia yake ya uzinzi lakini hakusikia la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Matendo haya ya Sulubu yalisababisha akaambukizwa maradhi ya UKIMWI. Sulubu hatimaye alimwambukiza mkewe Pendo na Rehema ambao waliaga dunia kutokana na athari ya ugonjwa wa UKIMWI.

Mhusika Fumbwe katika riwaya ya *Kala Tufaha* anapata ugonjwa wa UKIMWI kutokana na ukosefu wake wa uaminifu katika ndoa. Ndoa ya Fumbwe haikuwa na uaminifu kwa vile mkewe Hatima pia alikosa uaminifu katika maisha yake ya ndoa. Jamii ya Fumbwe ilikuwa na shida kubwa kwa maana mke na mume walikosa kuishi maisha ya uaminifu. Inaonekana wazi kwamba ndoa kati ya Hatima na Fumbwe inavunjika kwa sababu wote hawakuwa waaminifu.

Mwandishi anasema, "*Malipo yake kumla kivuli tena nyumbani kwake. Ndiyo na yeye alikuwamo na jicho la nje."*(Kala Tufaha, uk. 126). Fumbwe alimbaka Kibibi na kumpachika mimba Hatima anapokwenda kuzuru wazazi wake kule kijijini. Kibibi alikuwa ameenda kwa Fumbwe kusaidia kufanya kazi ya uyaya. Fumbwe kwa upande wake alimfumania Hatima akiwa na Chongea alipomhadaa Hatima kuwa ameenda kuwazuru wazee wake kijijini. Tukio hili lilimfanya Fumbwe kuachana na Hatima na kuanza kujiingiza katika ulevi na uasherati uliochangia hatimaye kumwambukiza maradhi ya UKIMWI. Ukosefu wa uaminifu katika ndoa ni tendo hatari kwa maana laweza kuivunja ndoa au kusababisha maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa.

Katika hadithi ya *Likizo ya Mauti*, msanii anayasawiri maisha ya Mzee Gogo ambaye pia alikuwa ameoa akiwa na jamii. Mzee Gogo alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na msichana mdogo aliyejulikana kama Ulimbo. Mzee huyu alimchukua msichana Ulimbo na akampeleka kwa likizo nje ya nchi. Mzee Gogo aligharamika sana ili kuhakikisha kuwa kipenzi chake kinafurahia likizo ya mbali. Mzee Gogo alijihusisha katika uhusiano wa kimapenzi na msichana ambaye umri wake haukuwa halali. Ziraili lilimnasa Mzee Gogo kwa sababu baada ya starehe zake zote na kipenzi chake, alianza kujuta kwa kupuuza ushauri aliokuwa amepata. Aliupata ugonjwa wa UKIMWI ulioanza kumla na hivyo kuiletea jamii yake madhara makubwa na aibu kuu.

Waandishi wa kazi teule zilizotumiwa wanaangazia ndoa hizi kwa lengo la kuwaonya wanajamii dhidi ya tabia ya uasherati. Katika kufanya hivyo, wanahimiza uaminifu katika ndoa kama njia ya kuepuka kuambukizwa maradhi

ya UKIMWI kwenye ndoa. Katika kuyashadidia maoni haya, wanaharakati wote wanaoshughulika katika kukabiliana na maradhi ya UKIMWI wanasisitiza kuhusu uaminifu katika ndoa. Wazo hili limeungwa mkono na asasi za kidini ambazo zinasisitiza uaminifu katika ndoa kama njia bora ya kudhibiti kuenea kwa maradhi ya UKIMWI.

**Kupinga Taasubi za Kiume**

Waandishi katika maandishi teule wanakashifu taasubi za kiume kama njia inyayofanya maradhi ya UKIMWI kuenea. Katika riwaya ya ***Ua la Faraja***, Ngoma anamdunisha mke wake kiasi cha kumwambukiza maradhi haya. Ngoma alikuwa tajiri kutokana na biashara yake lakini hakuutumia utajiri huo kwa manufaa ya jamii yake. Ngoma alipata pesa nyingi kutokana na biashara yake lakini alizitumia tu kwenye anasa. Alikunywa pombe akiwa na wanawake kama vile Queen na Asha na aghalabu alifika kwake usiku wa manane bila kumwogopa mkewe Tabu. Utajiri huu ulimpa Ngoma kiburi akamdharau mkewe kwa kuwa hakuwa na mapato yakilinganishwa na aliyoyapata Ngoma katika biashara yake. Taasubi za kiume zilimfanya Ngoma kumdharau mke wake kiasi cha kufanya mapenzi na wanawake wengine na kurudi nyumbani akiwa amelewa na kunukia marashi ya wanawake wengine. Katika kufanya maamuzi kuhusu jamii yao, tunaona Ngoma ndiye aliyehusika. Kwa mfano, Ngoma ndiye aliyefanya Tabu kuacha dini yake ya Kikristo na kujiunga na Uislamu. Aidha, katika kufanya mapenzi, yeye ndiye anayeamua kutumia mipira. Hii inajidhihirisha pale Ngoma anapomlaghai Tabu kuwa watu, hata wanandoa hutumia mipira. Ngoma anayafanya haya yote wakati alipokuwa amesikia fununu kuwa Queen alikuwa anaugua ugonjwa wa UKIMWI.

Katika riwaya ya *Pendo katika Shari*, mwandishi anamchora mhusika Sulubu akiiendeleza taasubi ya kiume. Sulubu aliamini kuwa UKIMWI ni ugonjwa wa wanawake na yeye kamwe hangeweza kuwa na ugonjwa huo. Hali hii ilimfanya hata kukataa kupimwa ili kuijua hali yake. Sulubu aliamini kuwa UKIMWI ni ugonjwa wa wanawake na hivyo hakuona sababu ya kupimwa ili kuthibitisha iwapo alikuwa na virusi vya UKIMWI au la. Sulubu alisisitiza kuwa haingewezekana kupatwa na ugonjwa wa UKIMWI kwani aliamini kuwa wanawake tu ndio wanaoambukizwa magonjwa kama hayo. Mtazamo kama wa Sulubu ni wa kusikitisha kwa maana hakuna magonjwa ambayo yaweza kuwa ya jinsia moja tu. Wanaume wengi waliofungwa na minyororo ya utamaduni waliamini kuwa chochote kibaya katika jamii kilitokana na wanawake. Wanaume wengine hutembea kwa njia mbaya na wanapopata magonjwa, huwa wanawalaumu wanawake kuwa chanzo cha magonjwa hayo. Tabia hii ya ubabadume ndiyo inayochangia kuendeleza ugonjwa wa UKIMWI katika jamii ambapo wanaume hujiona kuwa na uhuru wa kufanya lolote kama kufanya uzinifu nje ya ndoa.

Kwenye riwaya ya *Kala Tufaha*, ubabadume wa mhusika Fumbwe unamfanya kujihusisha na tabia ya uasherati inayosababisha apate maradhi ya UKIMWI. Alihusika katika kumbaka Kibibi aliyekuwa yaya wao na aidha alikuwa akijihusisha na vitendo vya uzinifu na wasichana wadogo kwenye afisi yake kazini. Fumbwe anafurahia baada ya kumfumania mke wake kwa vile waliachana hatimaye. Aliona kuwa sasa alikuwa amepata uhuru wa kufanya anasa lakini tabia yake ya uzinifu illimletea maradhi ya UKIMWI.

Onyango (2007) anaunga mkono wazo kuwa taasubi ya kiume ni kikwazo kikubwa katika vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI. Anashikilia kwa nguvu na itikadi za jamii zinaelekea kuwapendelea wanaume na katika hali hii wanawake ndio wanaoathirika kuhusiana na maambukizi ya UKIMWI. Hii inatokana na misingi ambayo inawapendelea wanaume na kuwadhalilisha wanawake. Waandishi wa kazi teule za riwaya waelekea kuukashifu ubabadume kama njia inayochangia kuenea kwa maradhi ya UKIMWI. Tabia hii ikikomeshwa, itachangia pakubwa katika kupunguza maambukizi ya UKIMWI miongoni mwa wanawake katika jamii. Licha ya vita dhidi ya taasubi za kiume, unyanyapaa hauna budi kupigwa vita iwapo tunataraji kushinda vita dhidi ya UKIMWI. Sehemu ifuatayo inajadili namna vita dhidi ya unyanyapaa vyaweza kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI.

**Kupinga Unyanyapaa**

Mwandishi wa riwaya ya *Ua la Faraja* anaangazia vita dhidi ya unyanyapaa kama njia nyingine ya kukabiliana na maradhi ya UKIMWI. Uvumbuzi wa maradhi ya UKIMWI uliitatiza jamii kabla ya kudhibitiwa na kueleweka kama maradhi yanayofanya mwili kupunguza kinga ya maradhi. Katika nyakati za mwanzo kulikuwa na semi tofauti zilizotumika zikayafanya maradhi haya yatishe. Baadhi ya watu waliuita uchawi, kifo, laana, ugonjwa mpya usio na tiba na kadhalika. Utambuzi wa ugonjwa wa UKIMWI kwa matumizi ya msamiati uliotajwa ulifanya walioathirika kuhisi kunyanyapaishwa. Baada ya utafiti wa kina kufanywa, wanajamii walipata ufahamu wa kutosha kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Wasanii wa kazi teule za riwaya wanakashifu chuki dhidi ya waliougua na kuhimiza upendo pamoja na kuwafurahia waathiriwa kama njia ya kupiga vita unyanyapaa.

Katika jamii zetu, kuna watu ambao wana mtazamo hasi kwa waathiriwa wa ugonjwa wa UKIMWI. Wao huwatenga na kuwabagua wagonjwa wa UKIMWI na matendo kama haya huwaathiri wagonjwa kwa njia hasi. Wagonjwa kama hawa huhisi kuchukiwa na huathirika kisaikolojia kiasi cha kuwafanya wasiishi maisha marefu. Tabia kama hii huendeleza unyanyapaa lakini mtunzi wa riwaya ya *Ua la Faraja* anapendekeza tuupinge unyanyapaa ndipo tuwape wagonjwa muda wa kuishi zaidi. Msanii anapendekeza upendo kama wa Daktari Hans kama njia ambayo pia inaweza kutumika katika kupambana na virusi vya ugonjwa wa UKIMWI. Licha ya upendo katika vituo vya afya na matibabu, jamii kule

nyumbani zinapaswa kuwa katika mstari wa mbele katika kuonyesha upendo kwa maana hapo ndipo mwathirika hukaa kwa muda mrefu.

Katika riwaya ya *Kala Tufaha*, mhusika Fumbwe alipolazwa hospitalini, Daktari Kala alimhudumia vyema kwa kumwonyesha upendo na kumjali sana. Fumbwe alihisi kupendwa na kufarijika mpaka akaufungua moyo wake kwa Daktari Kala. Ni sadfa kuwa Kala alikuwa amekutana na babake na kumhudumia pasipo kujua kuwa yeye ndiye babake. Fumbwe alipolazwa hospitalini baada ya kulemewa na ugonjwa, alipata huduma ya kipekee kutoka kwa Daktari Kala. Kala hakukosa hata siku moja kumpitia mgonjwa wake na kumjulia hali. Alijaribu sana kila siku, awe kazini au akose kuwa kazini kupata wasaa wa kumpitia mgonjwa wake na kumjulia hali. Hata akiwa safarini huwapigia wenzake simu ili kumjulia hali mgonjwa wake.

Mwandishi anatoa wito kwa huduma bora ya kuwajali wagonjwa kutoka kwa madaktari na wauguzi kama njia bora ya kupiga vita unyanyapaa. Tunaonyeshwa namna Fumbwe anavyoshughulikiwa na Daktari Kala na hivyo mwandishi anawataka madaktari wote waige mfano wa daktari huyu kwa kuwashughulikia wagonjwa huku wakiwaonyesha upendo. Kupitia mbinu hii, unyanyapaa utapigwa vita na tutafaulu katika vita vyetu dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI. Kama njia ya kuonyesha upendo kwa wagonjwa wao, tunaona Daktari Hans na Kala wakijiweka katika tajriba ya wahusika, wanawazia maisha yao, wanaweka fikra na hisia zao pamoja nao na kuanza kuandika sura mpya ya maisha ambayo msuko wake umetibuliwa na maradhi haya.

Katika riwaya ya *Pendo katika Shari*, mwandishi anaonyesha namna jamaa ya Sulubu inavyomwonyesha upendo wakati ambapo alikuwa amelazwa hospitalini. Licha ya madhila ambayo Sulubu alikuwa ameifanyia aila yake, wakati wanapotambua kwamba anaugua ugonjwa wa UKIMWI, wanamshughulikia kwa upendo na kumpa matumaini. Jamii haikutaka kulipiza kisasi lakini badala yake ikaonyesha upendo mkuu kwa Sulubu alipougua maradhi ya UKIMWI.

Kwa mshangao wa Sulubu, watoto na mke wake walimpa moyo na kumfariji. Watoto walimtembelea Sulubu hospitalini na wakamueleza kuwa wanampenda. Walimueleza kuwa walifahamu alikuwa anaugua ugonjwa wa UKIMWI lakini walimhakikishia kuwa akiishi maisha mazuri na kula vizuri hataweza kuteseka. Sulubu hakutarajia haya akikumbuka mateso ambayo alikuwa ameipatia jamii yake. Mwandishi anatusihi tusahau tofauti zetu na kuwashughulikia wagonjwa vyema na kwa njia hii tutawapa matumaini ya kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI kwa ujasiri mkuu. Sulubu alihisi upendo wa familia yake licha ya maovu yote aliyokuwa amewafanyia.

Mwandishi wa hadithi ya "Tahadhari Bandia" anapendekeza kwamba njia ambayo inaweza kutumika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI ni kupinga

unyanyapaa. Kwa mujibu wa hadithi hii, unyanyapaa unasababisha jamii kuwatenga na kuwadhulumu waathiriwa wa UKIMWI. Hali hii huwaathiri wagonjwa wengi kisaikolojia na hata kusababisha wengi wao kupoteza maisha yao mapema sana. Asasi mbalimbali za jamii kama vyuo vya mafunzo, mashirika ya serikali na yasiyo ya serikali yanapaswa kuwakubali wagonjwa wa UKIMWI kama wagonjwa wengine na kuepuka kuwatenga. Iwapo wagonjwa wa UKIMWI watachukuliwa kama watu wa kawaida pasipo kuwabagua, wataendelea kuishi kwa muda mrefu na kutekeleza majukumu mbalimbali kama raia wengine. Hili litawapa matumaini ya kuendelea kuishi. Licha ya kupinga unyanyapaa, elimu na mafunzo kuhusu UKIMWI ni muhimu katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI. Sehemu inayofuata inashughulikia elimu na mafunzo kama njia ya kupambana na UKIMWI.

**Kutoa Elimu na Mafunzo**

Njia nyingine ambayo inaweza kutumika katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI ni jamii kuhakikisha kwamba vijana wanapata elimu na mafunzo ya kijinsia kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Baadhi ya wazazi hawachukui jukumu la kuwapa watoto wao mafunzo. Baadhi yao husingizia dini na mila kuwa kizuizi kwao. Katika tamthilia ya *Kilio Chetu*, mwandishi anaonyesha athari ya kukosa elimu. Anaonyesha namna ambavyo vijana wanaangamia kwa kukosa maelezo na ufahamu kuhusu masuala yanayowaelekeza kujiingiza kwa uasherati unaowaletea mauti.

Mtunzi anaeleza, "*Basi watoto wakaendelea kudhoofika kwa kukosa elimu ya jinsia, Dubwana lile likaendelea kuwadhuru, wakateketea. Vifo vikawazoa… Vikawazoa…vikawazoa*." (Kilio Chetu, uk. 3). Mwandishi anasema kuwa, dubwana ambalo ni ugonjwa wa UKIMWI limeendelea kudhuru na kuangamiza maisha yao. Inabainishwa kuwa vifo vingi sana vimetokea miongoni mwa vijana kwa sababu ya ukosefu wa elimu kuhusu UKIMWI. Mwandishi anapendekeza kwamba njia bora ya kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI ni kwa vijana kupewa elimu ya familia, ikiwemo ya jinsia. Watoto wanapaswa kuelezwa wazi kuhusu masuala ya mapenzi, ngono na hatima yake. Elimu inayopendekezwa inalenga kuwaonyesha vijana na watoto madhara ya kufanya ngono kabla ya ndoa.

Mwandishi wa tamthilia ya *Giza* anatueleza kuwa wanaohusika na hasa viongozi serikalini hawajatoa elimu na mafunzo ya kutosha kuhusu UKIMWI. Ni jukumu la viongozi walio mamlakani kuhakikisha kuwa wanayashughulikia maslahi ya raia wao. Katika jamii inayorejelewa inaonekana kwamba viongozi wamezembea kazini badala ya kuwajibika. Mtunzi anawakashifu viongozi serikalini kwa kutowajibika kuhusu uhamasishaji wa jamii dhidi ya UKIMWI. Katika tamthilia ya **Giza**, mtunzi analalama kuwa, " *madawa na huduma kuhusu UKIMWI zinaishia katika sehemu za mijini. Wanachojua ni kula pesa nakuimba maredioni na majukwaani juu ya kondomu.*" (Giza, Uk. 18). Serikali imewasahau

watu wa sehemu za vijijini kwa kukosa kuwapa madawa na elimu kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Vingozi wanaohusika wanasahau kuwa katika sehemu za mashambani kuna watu wengi sana ambao wanakosa elimu na ufahamu kuhusu ugonjwa wa UKIMWI.

**Kuzingatia Maadili ya Jamii**

Maadili ni tabia au mwenendo bora unaokubalika kuzingatiwa na jamii husika. Mwandishi wa tamthilia ya *Giza* anatueleza kwamba njia bora ya kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI ni kuzingatia maadili mema katika jamii. Vijana wa Vyuo Vikuu wanapaswa kujiepusha na tabia ya kujihusisha na mapenzi kiholela ili waepuke kuupata ugonjwa wa UKIMWI. Vijana wengi katika tamthilia ya *Giza* wamesawiriwa kuwa na wapenzi wengi na jambo hili linahatarisha maisha yao. Uwezekano wa kuupata ugonjwa wa UKIMWI uko juu sana iwapo mhusika atafanya ngono na watu wengi. Aidha, mwandishi anatueleza kwamba, kama mtu amepatwa na ugonjwa wa UKIMWI, si vyema kuusambaza kimakusudi kwa wengine.

Msanii anatuonyesha namna ambavyo mhusika Mona amejiingiza katika kusambaza ugonjwa wa UKIMWI kwa kufanya mapenzi na yeyote aliyekuwa tayari. Mona hayazingatii maadili. Mtunzi anasema, "*Mbona nishanasa wengi wanajigonga tu. Siachi vitu, mbona mimi pia hawakunihurumia?*" (Giza, uk. 29-30). Mona anadai kufanya hivyo kwa maana anasema kuwa yeye pia hakuhurumiwa ndipo akaupata ugonjwa wa UKIMWI. Kutokana na dondoo lililo hapo juu, tunaona kwamba tabia ya Mona ni ya kulipiza kisasi. Mona ameamua kuwa hawezi kuangamia peke yake. Tabia ya mhusika huyu inakiuka maadili ya jamii.

Mwandishi wa hadithi fupi ya "tahadhari bandia" anatoa pendekezo lingine la kupambana na ugonjwa wa UKIMWI. Katika hadithi hii, msanii anatueleza kuwa sheria za kitaaluma hazikuruhusu kuyatangaza matokeo ya uchunguzi wa mara ya kwanza kabla ya kuyadhihirisha na kuyathibitisha. Baadhi ya madaktari katika hadithi hii wanayatangaza matokeo kwa mgonjwa kabla ya kuthibitishwa. Matokeo kama haya yanaweza kudhuru maisha ya mtu kisaikolojia. Mhusika Wakesho aliathirika vibaya sana mpaka akaanza kutengwa na jamii kwa kutuhumiwa kuwa na virusi vya UKIMWI. Uchunguzi zaidi ulipofanywa, ilitokea kwamba Wakesho hakuwa na virusi vya UKIMWI.

Mtunzi anapendekeza kwamba wauguzi na madaktari wanapaswa kumakinika katika utekelezaji wa majukumu yao. Wafanyakazi hawa ni wa umuhimu mkubwa katika maisha ya wagonjwa. Kauli zao na matendo yao yanaweza kuyaponya ama kuyaangamiza maisha ya wagonjwa. Mwandishi anapendekeza kuwa wafanyakazi sharti wafuate sheria na maadili ya kazi hasa kwa kutoa matokeo ya uhakika kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Aidha, namna

ambavyo matokeo yanatangazwa inaweza kumpatia mwathiriwa matumaini ya kuishi ama kumgongea msumari wa mwisho juu ya jeneza lake.

## Hitimisho

Kazi hii imejadili kwa kina namna ambavyo maandishi teule ya fasihi andishi yametumika katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI. Baadhi ya njia zilizopendekezwa kupambana na UKIMWI ni pamoja na kuepukana na uasherati, kupinga unyanyapaa, kuzingatia maadili katika jamii na kuwa waaminifu katika maisha ya ndoa miongoni mwa zingine. Kufikia sasa, wataalamu wa tiba hawajafanikiwa kupata dawa inayoweza kutibu ugonjwa wa UKIMWI. Wasomi na watafiti wanapaswa kuchukua jukumu la kuwasilisha ujumbe ulio kwenye maandishi mbalimbali ya fasihi katika warsha na makongamano ili jamii ifahamishwe kuwa, licha ya huduma za kimatibabu, kuna njia mbadala ambazo zaweza kutumika kupambana na ugonjwa wa UKIMWI.

## Marejeleo

Iribemwangi, P. I. (2007). *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Jilala, H. (2004). *Giza*. Bukoba: Angaza Initiative Company Ltd.

Kathenya, M. (2002). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Islands: Augustine College.

King'ei, K., & Kobia, J. (Wahariri) (2007). *Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Matundura, B. (2008). *Sitaki Iwe Siri*. Nairobi: Longman Publishers.

Medical Aid Foundation. (2010). *Kilio Chetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House Ltd.

Mkufya, W. E. (2005). *Ua la Faraja*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T) Ltd.

Momanyi, C. (2008). *Pendo Katika Shari*. Nairobi: Longhorn Kenya Publishers.

Omar, B. (2005). *Kala Tufaha*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Mutembei, A. K. (2009). *UKIMWI Katika Fasihi ya Kiswahili, 1992-2006*. Dar es Salaam: TATAKI.

Mutembei, A. K. (2001). *Poetry and HIV AIDS in Tanzania: Changing Metaphors and Metonymies in Haya Oral Traditions*. Leiden University: Leiden University: CNWS Publications. Vol 101.

Mutembei, A. K., na Wengine (2002). Communicating about HIV/AIDS - Changes in Understanding and Coping with help of Language in Urban Kagera, Tanzania. *Journal of Asian and Africana Studies*, 37(1), 1-6.

Reynolds, S. (2006). *Orodha*. Dar es Salaam: Macmillan Adan.

Thavis, J. (2009). "*Pope's Condom Comments latest Chapter in Sensitive Church Discusion*" http://www.catholicnews.com/data/stories/cns/0901232.htm.7/10/2011

UNAIDS. (2012). World Aids Day. *The Standard*, Tuesday, December 4 2012. Nairobi: Standard Media Group.

Walibora, K., & Mohamed, S. (2010). *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd.